HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA MAADHIMISHO YA MIAKA 20 YA BARAZA LA AMANI NA USALAMA LA UMOJA WA AFRIKA, TAREHE 25 MEI 2024, UKUMBI WA KIMATAIFA WA MIKUTANO WA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM

Mheshimwia Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

Waheshimiwa Wawakilishi wa Wakuu wa Nchi na Serikali;

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali Wastaafu;

Mheshimiwa Olusegun Obasanjo, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria;

Mheshimiwa Domitien Ndayizeye, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Burundi;

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Moussa Faki Mahamat, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika;

Mheshimiwa January Makamba (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;

Waheshimiwa Mawaziri mliopo hapa;

Waheshimiwa Wawakilishi wa Kudumu wa Nchi wajumbe wa Baraza la Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika;

Mwenyeji wetu, Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Mheshimiwa Balozi Bankole Adeoye, Kamishna wa Masuala ya Siasa, Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika;

Mheshimiwa Balozi Said Djinnit, Kamishna wa Kwanza wa Masuala ya Siasa, Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Habarini za asubuhi?

Ndugu Viongozi, Mabibi na Mabwana, leo imetimia miaka 20 tangu kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika. Baraza hilo lina jukumu la kuzuia, kudhibiti na kutatua migogoro katika bara letu.

Hivyo, nikiwa Mwenyekiti wa Baraza la Amani na Usalama kwa kipindi cha mwezi wa Mei 2024, ninayo furaha kuwakaribisha Dar es Salaam, Tanzania, katika Maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa Baraza hili. Ninawapongeza sana wote waliofanya maandalizi ya maadhimisho haya, ***hongereni sana!***

Pia, kama mnavyojua, kila tarehe 25 Mei, Bara la Afrika huadhimisha Siku ya Afrika. Hivyo nitumie fursa hii pia,

kuwatakia ***nyote kheri ya Siku ya Afrika***. Kama ilivyokuwa tangu enzi za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, napenda kuwahakikishia kwamba, Tanzania itaendelea kutoa kipaumbele katika kuhakikisha kuwa Umoja wetu unafikia malengo tuliyojiwekea. Hakika, historia ya mafanikio yetu katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, lazima itupe hamasa katika jitihada zetu za sasa za kulinda amani, kujiletea maendeleo na kuhakikisha ustawi wa watu wetu.

Waheshimiwa Viongozi,

Pamoja nasi, tumepata heshima ya kuungana na Mheshimiwa Olusegun Obasanjo, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria. Mnamo tarehe 25 Mei 2004, Mheshimiwa Obasanjo alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa kwanza kabisa wa Baraza la Amani na Usalama. Akiwa ni kiongozi ambaye ameliona Baraza hili likifanya kazi kwa miaka mingi hadi leo, tunatazamia kusikia na kujifunza mengi kutoka kwake na kupata busara zake pia. Mbali na Mzee Obasanjo, tupo na viongozi wengine wastaafu ambao kama inavyonekana kwenye mpangilio wa shughuli za leo, tutawasikia wakitoa maoni yao kuhusu Baraza hili.

Tunaye Mheshimiwa Domitien Ndayizeye, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Burundi, ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Wazee wa Umoja wa Afrika.

Tunaye pia Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye

alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje wakati Baraza linaanzishwa na kama Rais pia kwa nyakati tofauti alikuwa Mwenyekiti wa Baraza hili.

Vile vile tunaye Mheshimiwa Said Djinnit, Kamishna wa kwanza wa Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika, aliyepewa jukumu la kuwezesha Baraza hili lianze kufanya kazi.

Nitumie fursa hii pia kuzipongeza Nchi Wanachama wapya 10 waliojiunga na Baraza hili kuanzia mwezi Aprili mwaka 2024, na kuwaahidi ushirikiano wetu.

Ndugu Viongozi na Wageni Waalikwa,

Wakati Baraza hili likiadhimisha miaka 10 ya kuanzishwa kwake, mwezi Mei 2014, kama ilivyo sasa, Tanzania pia ilikuwa Mwenyekiti wa mwezi wa Baraza hili. Hata hivyo, hafla rasmi ya kuadhimisha miaka 10 ilifanyika mwezi Juni 2014 nchini Equitorial Guinea, ambapo Mwenyekiti wa Mwezi kwa wakati huo, alikuwa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, na ndiye aliyeongoza Maadhimisho hayo. Hivyo basi, ninafarijika kwamba mara hii, miaka 10 baadaye, Tanzania sio tu ni Mwenyekiti wa Mwezi wa Baraza hili, lakini pia imepata fursa ya kuwa nchi mwenyeji wa Maadhimisho ya kutimiza miaka 20 ya Baraza hili.

Waheshimiwa,

Maadhimisho haya yamepewa Kaulimbiu isemayo ***"Miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa***

Afrika kama Chombo cha Kudumu cha Maamuzi: Miongo Miwili Ijayo ya Amani na Usalama ya Afrika Tuitakayo". Kaulimbiu hii inatutaka kufanya tathmini ya safari yetu tangu kuanzishwa kwa Baraza hili hadi sasa, na kutafakari kwa kina tuendako. Baada ya miongo miwili ya uwepo wa Baraza, tumejifunza nini, na ni mikakati ipi tunapaswa kuiweka ili kuhakikisha tunakuwa na Afrika tutayoitaka yenye amani katika miongo miwili ijayo?

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza la Amani na Usalama limekuwa na nafasi muhimu katika kukuza amani, usalama, na utulivu katika bara letu la Afrika. Mnamo tarehe 26 Disemba 2003, Itifaki ya kuanzisha Baraza hilo ilianza kutekelezwa kufuatia kuridhiwa na Nchi Wanachama 27 wa Umoja wa Afrika. Hadi kufikia mwezi Mei 2004 wakati Baraza lilipofanya kikao chake cha kwanza, Nchi Wanachama 32 zilikuwa zimeiridhia Itifaki hiyo. Leo hii, nafurahi kusema kwamba, Nchi Wanachama 53 zimekwishairidhia Itifaki hiyo, kati ya nchi 55 za Umoja wa Afrika. Hii inadhihirisha kwamba, Nchi Wanachama zinatambua kuwa Baraza hili lina nafasi muhimu sana katika kuleta amani na usalama barani Afrika.

Miaka 20 iliyopita, wakati chombo hiki kinaanzishwa, kilipewa dhima ya kiutendaji katika kushughulikia migogoro kwa ufanisi, na kuimarisha uwezo wa kuleta amani, usalama na utulivu kote barani Afrika. Ilifanywa hivyo kwa kutambua nafasi hasi ya vita na mapigano katika kurudisha nyuma maendeleo ya jamii. Tangu kuanzishwa kwake, Baraza

limepata mafanikio mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuanzisha majadiliano ya upatanishi hadi kusaidia nchi kujengwa upya baada ya vita (*post-conflict reconstruction and development*).

Baraza pia limekuwa na mchango katika kukabiliana na migogoro na matishio mbalimbali ya kiusalama. Kutoka Sahel hadi Somalia, Baraza limechangia juhudi za Bara letu katika kukabiliana na ugaidi. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Baraza limejidhatiti kusimamia misingi ya haki za binadamu, demokrasia na utawala bora. Vile vile, limeangazia masuala ya ushirikishwaji wa wanawake na vijana kwenye masuala ya amani na usalama na hivyo kutambua nafasi muhimu ya wanawake na vijana katika ujenzi wa amani.

Katika ngazi ya Kitaifa, Baraza limeshirikiana na nchi zinazokabiliwa na changamoto za amani na usalama, na kufanya ziara katika nchi hizo (field missions). Ziara hizo zimeliwezesha Baraza kuelewa vyema zaidi changamoto za kiusalama, kusikiliza kutoka kwa wanaohusika na wanaosibiwa na migogoro hiyo, na kuonesha mshikamano na waathirika wa migogoro.

Kikanda, Baraza linaendelea kushirikiana na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ili kuimarisha uratibu wa jitihada za amani na usalama na kubadilishana uzoefu.

Baraza hili, limekuwa pia na mashirikiano ya kitaasisi na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Kamati ya Siasa na

Usalama ya Umoja wa Ulaya na hivyo kuongeza ushawishi wa Bara la Afrika duniani. Tunayo kila sababu ya kupongeza juhudi za Wajumbe watatu wa Afrika kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (A3), hususan katika kutetea misimamo ya pamoja ya Umoja wa Afrika katika ajenda za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Mwaka jana, tumeshuhudia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa likiridhia wito wa muda mrefu wa Umoja wa Afrika kuhusu operesheni za kulinda amani za Umoja wa Afrika kupata ufadhili wa Umoja wa Mataifa, hatua ambayo ni muhimu katika kuhakikisha kunakuwa na uwezo endelevu na hali inayotabirika wa rasilimali kwa ajili ya misheni hizo za Umoja wa Afrika.

Nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili na Kamisheni, akiwemo Mwenyekiti, Kamishna wa Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama, Sekretarieti ya Baraza la Amani na Usalama na washirika wote ambao wamechangia kufanikisha kazi ya Baraza hili tangu kuanzishwa kwake.

Waheshimiwa Viongozi,

Licha ya mafanikio haya, bado kuna changamoto. Tunashuhudia mapigano kwenye baadhi ya maeneo, matukio ya uhalifu unaovuka mipaka, na kukosekana kwa mifumo inayotumia viashiria vya tahadhari ili kuzuia migogoro. Kwa ujumla, ***bado hatujaweza kunyamazisha kabisa bunduki*** barani Afrika.

Changamoto nyingine kubwa ni kuzuka upya kwa wimbi la mabadiliko ya serikali kinyume na katiba, na kukwama kwa michakato ya kurejesha utawala wa kiraia kwa mujibu wa katiba. Kujirudia kwa changamoto hizo kunaibua maswali makubwa mawili; kwa nini changamoto hizi zinaendelea? na je tunasimamia ipasavyo kanuni zetu kuhusu masuala haya? Itafaa Kongamano hili likatusaidia kupata majibu ya maswali haya.

Ndugu Waafrika wenzangu,

Sanjari na hayo, viongozi waliotangulia kabla yetu kama Rais Obasanjo, watakubaliana nami, kwamba, kuna mabadiliko ya aina ya migogoro na aina ya vitisho vinavyolikabili bara letu kwa sasa. Pia, yapo masuala ambayo yamekuwa yakijirudia kwenye agenda ya Baraza bila kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kwa maoni yangu, hali hii haiendani na dhamira ya viongozi wetu wakati wanaanzisha Baraza hili.

Ni kwa mnasaba huo, mjadala huu na michango yenu ni muhimu sana, hususan katika muktadha wa kujifunza kwa historia na kujipanga kwa siku zijazo. Naamini, mambo mengi yatajadiliwa na washiriki waliopo hapa, ikiwemo viongozi na wataalam mbalimbali. Kwa upande wangu, ningependa kugusia masuala machache, nikijikita katika **kuimarisha uwezo wa kuthibiti migogoro, kutumia kikamilifu nyenzo zilizopo na kuimarisha ushirikiano na wadau.**

Kuhusu diplomasia ya kuzuia na kusuluhisha migogoro, ni dhahiri kwamba, funzo kubwa ni kwamba kinga ni bora kuliko tiba, lakini zaidi, kinga ni suala endelevu. Hivyo, hatuna budi kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema na mifumo ya kuzuia migogoro. Tunahitaji pia kuweka kipaumbele katika michakato ya mazungumzo, upatanishi na maridhiano ambayo ni jumuishi. Itasaidia sana kwa Baraza hili kujikita zaidi kwenye hali halisi ya nchi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yake na inapobidi kuingilia kati kuisaidia nchi husika katika utekelezaji wa maamuzi ya Baraza.

Kuhusu nyenzo za Umoja wa Afrika, kwa sasa tunayo miongozo/nyenzo muhimu ambazo bado haitumiki kikamilifu katika kulisaidia Baraza kutimiza wajibu wake. Ni imani yangu kwamba, matumizi kamili ya miongozo hiyo, ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Umoja wa Afrika kuhusu Kunyamazisha Silaha barani Afrika ni muhimu katika kuelekeza juhudi zetu za kukuza amani na usalama. Ni lazima pia tuhakikishe Jeshi la Utayari la Afrika na Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika inafanya kazi na kutumika ili kuongeza uwezo wetu wa kutekeleza mipango yetu ya usalama.

Kuhusu ushirikiano na wadau mbalimbali, tunatambua kwamba ushiriki wa wanawake na vijana kwenye mazungumzo ya amani na jumuiya za kikanda ambapo migogoro imetokea ni muhimu katika utafutaji wa amani. Tuendako, Baraza linapaswa kuwawezesha wanawake na vijana kama mawakala wa kuleta mabadiliko chanya.

Tunapaswa kuwekeza zaidi katika kuimarisha uratibu na ushirikiano wa kikanda. Pia tunatakiwa kuwekeza zaidi katika mipango ya kujenga uwezo na kukuza ustahimilivu kwa jamii zetu kwa ujumla, kwa kuwa migogoro mingine ina sababu za kihistoria baina ya watu wa makabila au makundi mbali mbali.

Kwa ujumla wake, tunahitaji pia kuimarisha ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa, kama vile Umoja wa Mataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Asasi za Kiraia kiraia, na washirika wengine wa maendeleo, ili kupata rasilimali na ujuzi kwa ajili ya afua imara za amani na usalama.

Mwisho, ninapenda kutoa wito kuhusu matishio mawili makubwa ya amani na usalama barani Afrika kwa sasa. Kwanza kabisa, ni ugaidi na itikadi kali vinavyozikumba kanda zote 5 za Umoja wa Afrika. Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika Mei 2022 jijini Malabo, Eqautorial Guinea ulitoa mwongozo kuhusu hatua madhubuti za kukabiliana na tishio hili. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa Azimio la Malabo linatekelezwa kikamilifu. Ni muhimu pia, kutafakari ni kwa jinsi gani tunaweza kushughulikia kwa upana wake, suala la ugaidi barani Afrika, ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia, na operesheni za pamoja.

Tishio la pili ni kuzuka tena kwa visa vya mabadiliko ya serikali kinyume na katiba. Ni nini kinachoruhusu kuzuka tena

kwa visa hivi? Kama Nchi Wanachama, ni lazima tuchukue hatua kulingana na maamuzi yaliyopitishwa na Baraza na kuhakikisha nchi zilizoathirika zinarejea haraka katika utaratibu wa kikatiba, huku pia tukishughulikia sababu kuu za mabadiliko hayo, yakiwemo mapungufu ya kiutawala na kukosekana kwa utulivu wa kisiasa.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana,

Kabla sijahitimisha, niwahakikishie kwamba, ni dhamira ya Tanzania kukuza amani na usalama barani Afrika ili kuweka mazingira stahiki ya kujenga ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa watu wetu. Nikimnukuu Hayati Nelson Mandela, "*amani ni kutengeneza mazingira ambapo kila mtu anaweza kustawi*." Bila shaka, jitihada za pamoja ni muhimu katika kukabiliana na changamoto za kiusalama zinazotukabili na katika kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ndani ya Bara letu la Afrika.

Baada ya kusema hayo, sasa, ninayo heshima kutamka kwamba Kongamano la Kuadhimisha Miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, limefunguliwa.

Asanteni kwa kunisikiliza.

African Union Commission (AUC)

PAPS Digital Repository **https://papsrepository.africa-union.org/**

Peace and Security Council General Collection

2024-05-25

Dar es Salaam Declaration on the 20th Anniversary of The African Union Peace and Security Council Held on 25 May 2024 in Dar es Salaam, Tanzania.

Peace and Security Council

African Union Commission

https://papsrepository.africa-union.org/handle/123456789/2101

Downloaded from PAPS Digital Repository, Department of Political Affairs, Peace and Security (PAPS)